**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA PILI

**29 JANUARI, 2020**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA PILI – TAREHE 29 JANUARI, 2020

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2019.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

### 12. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara za Mji wa Mafinga hazipitiki kwa mwaka mzima na kati ya kilomita 407 kwa mujibu wa DROMAS lami ni kilomita 5.58:-

Je, Serikali ipo tayari kuiongezea fedha TARURA ili ijenge barabara za kupitika kwa mwaka mzima.

### 13. MHESHIMIWA DEVOTHA MATHEW MINJA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara ya Mei Mosi – Nanenane katika Manispaa ya Morogoro imegharimu fedha nyingi sana za Serikali lakini barabara hiyo haikujengwa katika viwango vinavyofaa:-

Je, kwa nini Wakandarasi waliohusika na ujenzi wa barabara hiyo wasichukuliwe hatua.

## WIZARA YA MAJI:

**14. MHESHIMIWA BALOZI DKT. DIODORUS BUBERWA KAMALA (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini mradi wa maji kwa ajili ya Kyaka – Bunazi utaanza kutekelezwa.

**15. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mtandao wa maji Magu kupeleka Tarafa ya Ndagalu Kata za Shishani, Njinjinili, Kabila, Nkungulu, Ng'haya, Sukuma, Buhumbi na Mwamabanza zenye jumla ya Vijiji 24.

## WIZARA YA NISHATI:

**16. MHESHIMIWA FREDY ATUPELE MWAKIBETE (BUSEKELO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Katika eneo linalopatikana gesi aina ya *Carbondioxide* ($C_{02}$) kwenye Jimbo la Busekelo Kijiji cha Mpata kuna visima ambavyo ni hatari kwa binadamu na viumbe hai wengine kwani

huwa wanakufa wakivuta hewa ya sehemu hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru maisha ya binadamu na viumbe katika eneo hilo.

**17. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa Gridi ya Taifa Mkoani Katavi.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**18. MHESHIMIWA VEDASTO EDGAR NGOMBALE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Zoezi la kupeleka mifugo Mikoa ya Kusini limeleta madhara makubwa kwa mazingira na Wananchi kwa ujumla kwa sababu ya kukosa maandalizi kabla ya utekelezaji wa zoezi hilo:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kujenga Malambo ili kunusuru tatizo la maji kwa mifugo hiyo;

(b) Je, Serikali ipo tayari kuondoa mifugo iliyopo katika maeneo ambayo hayakupangwa kwa ajili ya mifugo kutokana

na mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Kata ya Mifola, Kandawale na Somanga.

**WIZARA YA KILIMO:**

**19. MHESHIMIWA ESTHER MICHAEL MMASI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Mfereji wa *Muo Irrigation Scheme* ni mradi wa umwagiliaji uliopata fedha takribani Shilingi millioni 248 mwaka 2018:-

Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kukamilisha mradi huo kwa faida ya wakazi wa Old Moshi Mashariki.

**20. MHESHIMIWA ENG. CHRISTOPHER KAJORO CHIZA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Mwaka 2005 Serikali ilikamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Itumbiko, lakini banio lake limeharibika na kusababisha Skimu nzima kushindwa kufanya kazi; Aidha, Serikali kupitia mfuko wa *"Food Aid Counterpart Fund"* ilipata Shilingi milioni 300 ili kujenga miundombinu ya Umwagiliaji katika Kijiji cha Gwanumpu lakini mradi huo hauendelei licha ya kutengewa fedha za utekelezaji:-

(a) Je, ni lini Serikali itakarabati banio la Skimu ya Umwagiliaji ya Itumbiko ili kuokoa miundombinu inayoendelea kuharibika na kuwasaidia Wananchi kuendelea kulima;

(b) Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kuwasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kakonko ili kufuatilia fedha za *Food Aid Counterpart Fund* ambazo zimekosa wafuatiliaji.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**21. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Wilaya ya Karatu ilipata mfadhili wa kujenga Chuo cha VETA na ujenzi umekamilika toka mwaka 2017 na tayari majengo yote yemekabidhiwa kwa Halmashauri:-

Je, ni lini sasa Serikali itakipa Chuo hicho usajili wa kudumu pamoja na mahitaji mengine kama ilivyo katika Vyuo vingine.

**22. MHESHIMIWA SUSAN LIMBWENI KIWANGA (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Jimbo la Mlimba lina

Wahitimu wengi wa Shule za Msingi na Sekondari ambao wanabaki majumbani kila mwaka :-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi ili Vijana hao wapate ufundi stadi na kuweza kujiajiri.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**23. MHESHIMIWA RICHARD PHILIP MBOGO (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Huduma za matibabu ya Madaktari bingwa zipo katika Kanda zote isipokuwa kanda za Magharibi na Kusini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hizo Mkoani Katavi ili kusaidia Wananchi wa Kanda ya Magharibi.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**24. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda biashara za wazalishaji wa ndani ili kuwajengea uwezo kuelekea uchumi wa Viwanda.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

**25. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Mwelekeo wa Serikali kwa sasa ni kuimarisha utalii wa picha badala ya utalii wa uwindaji kwenye Mapori ya Akiba nchini:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na lango la utalii wa picha katika Pori la Akiba la Selous ukanda wa Kusini kwenye Wilaya za Tunduru na Liwale.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**26. MHESHIMIWA ABDALLAH ALLY MTOLEA (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati Gereza la Keko ambalo miundombinu yake imechakaa sana.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Shughuli za Kamati hiyo kwa Mwaka 2019.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati hiyo kwa Mwaka 2019.

**DODOMA** **S. KAGAIGAI**
**29 JANUARI, 2020** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA